

Swali: Je Bwana Mungu anayo jinsia kama wanadamu tulivyo na jinsia?

Jibu: Biblia inasema Mungu alimwumba “**MTU**” kwa mfano wake, na si “**WATU**” kwa mfano wake.

Na Mtu wa kwanza kuumbwa alikuwa ni **ADAMU** mwenye jinsia ya **KIUME**, na baadaye ndipo Hawa akaumbwa kutoka katika ule ubavu uliotwaliwa kwa Adamu.

Kwahiyo Mtu wa kwanza kuumbwa aliyekamilika ndio **TASWIRA** kamili ya MUNGU. Na Mtu huyo ni Adamu, aliye na jinsia ya kiume,

Sasa maadamu MUNGU si mwanadamu, hivyo yeye hana jinsia ya kiume, bali anao **Utu wa KIUME**, Kwasababu jinsia inahusisha mambo mengi ya kibinadamu ikiwemo mifumo ya uzazi. Lakini Mungu yeye sio kama sisi wanadamu, hivyo yeye anao utu wa KIUME na sio wa KIKE, na utu huo wa Kiume alionao ulianza kwake ndipo tukapewa sisi, na haukuanza kwetu kisha yeye akaiga baadae hapana!

Hivyo kwa hitimisho ni kwamba utu wa MUNGU ni wa kiume, na ndio sababu anajitambulisha yeye kama BABA kwetu, (*Soma Mathayo 6:9*) na

sehemu nyingine anajitambulisha kama MUME (*Soma Isaya 54:5*), na hakuna mahali popote katika biblia panapoonyesha Bwana MUNGU akuchukua uhusika wa kike, au utu wa kike.

Na la mwisho pia kufahamu ni kuwa, Mungu ni Roho, na tunamwabudu katika Roho na kweli.

Yohana 4:23 "Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu

24 Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli."

Je umeokoka?, kama bado unangoja nini?..Hizi ni siku za mwisho na YESU yupo mlangoni, wakati wowote parapanda ya mwisho italia, je utakuwa wapi?

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako

bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

**Anaposema mwanamume mmoja katika elfu nimemwona
anamaana gani?**

NI KIPI MUNGU ANACHOKITAZAMA ZAIDI, MOYO AU MWILI?

Je shetani ana uwezo wa kujua mawazo ya mtu?

VIJANA NA MAHUSIANO.

Je suruali ni vazi la kiume tu?

Je Mungu ana jinsia?

Rudi Nyumbani

Share on:
WhatsApp